MONITORING LEARNERS PROGRESS

SASON 002

GREDI YA 4, MWAKA: 2021

KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amuulize mwanafunzi maswali yafuatayo.

1. Hujambo? _____
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Taja chakula ukipendacho. _____
   (Mwanafunzi ajibu)
3. Unajua kukipika chakula hicho? _____
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Chakula hicho hupatikana wapi? _____
   (Mwanafunzi ajibu)
5. Chumba cha kupikia chakula huitwaje? _____
   (Mwanafunzi ajibu)

Vigezo vya Kutathminia - Kusikiliza na Kuzungumza

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI (Alama 5)

Mwanafunzi asome kifungu hiki kwa sauti.

Juma alialikwa katika sherehe ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Ali. Aliamka asubuhi na mapema. Akaoga na akavaa nguo yake safi. Hakutaka kuchelewa hata kidogo. Viatu vyake pia vilikuwa safi ajabu. Alitembea polepole hadi kwa akina Ali.

Huko aliwapata watoto wengine. Kila mtu alikuwa mwenye furaha kuu. Hakika sherehe ilikuwa imeanza kunoga. Mamake Ali aliwaletea sharubati na biskuti. Walifurahia sana. Hatimaye keki ililetwa. Ali aliambiwa aikate huku watoto wenzake wakiimba. Kulikuwa na shangwe, vifijo na nderemo.

Vigezo vya Kutathminia - Kusoma

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Maneno yaliyosomwa katika dakika moja	60 na zaidi	41 - 60	21 - 40	0 - 20